**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI, MPANGO WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema na uzima na kuweza kukutana katika Baraza hili kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi wetu ambao wametutuma kwa kutuamini katika kusimamia hoja zao mbali mbali kwa maendeleo yao binafsi na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii pia kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Kukamilika kwa Hotuba hii na kufikia hatua ya kuisoma hapa leo, kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na mashirikiano ya karibu walionipatia Wajumbe wa Kamati yangu katika kupitia na kutoa michango yao. Hivyo, natumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati na naomba wazidi kunipa mashirikiano katika utekelezaji wa majukumu yetu mbali mbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 93(3) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la mwaka 2020) ambayo

yanaelekeza kuwa, Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa yatawasilishwa katika Kamati ya Bajeti kabla ya kuwasilishwa Barazani, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa, Kamati imeitekeleza vyema Kanuni hiyo kwa kufanya majadiliano na Afisi ya Rais - Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa kazi hii, Kamati pia ilizingatia Kanuni ya 93(4) inayotoa fursa kwa Kamati kuwaalika Wenyeviti wa Kamati za Kudumu pamoja na Wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao kuhusiana na Mapendekezo ya Mwelekeo wa Mpango wa Taifa na Bajeti ya Serikali. Kiujumla maoni yao yamesaidia sana katika kufanikisha kazi hii na kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kuwashukuru wote.

## TATHMINI YA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2021

### Ukuaji wa Uchumi

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonyesha kuwa, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar imeimarika na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 1.3 ya mwaka 2020. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii ambapo ukuaji huu umepelekea pia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya huduma, sekta ya fedha na sekta ya uwekezaji. Hatua hii imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na juhudi za Serikali katika kudhibiti maambukizi ya UVIKO 19.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inasisitiza juu ya ukuaji wa uchumi unaopelekea kupatikana kwa maendeleo ya kiuchumi na unaozingatia ukuaji wa sekta zinazowanufaisha wananchi wengi na kunyanyua pato la mtu mmoja mmoja. Aidha, upatikanaji wa ubora wa maisha ya watu katika nyanja mbali mbali ikiwemo elimu, afya na

makaazi bora kunatoa taswira njema kwa wananchi wetu na ndio uhalisia wa ukuaji na maendeleo ya kiuchumi wanakokutarajia.

## Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu za Pato la Taifa ni miongoni mwa viashiria muhimu vinavyosaidia katika kutathmini mwenendo wa uchumi kwa vipindi tofauti ikiwemo muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Pato la Taifa kwa mwaka 2021 limefikia thamani ya TZS 3,275 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 3,116 bilioni kwa mwaka 2020. Kamati inaipongeza Serikali kwa ukuaji huu na kusisitiza kuwa, takwimu hizi zitumike katika kufanya tathmini ya mabadiliko yanayotokea katika uchumi wetu na kuchukua hatua madhubuti kwa sekta ambazo hazikuonyesha kutoa mchango mkubwa ili hatimaye ziweze kuimarika.

## Mfumko wa Bei

**Mheshimiwa Spika,** Kasi ya Mfumko wa Bei za bidhaa na huduma nchini umepungua na kufikia wastani wa asilimia 1.7 kwa mwaka 2021 ikilinganishwa na wastani wa 3.4 kwa mwaka 2020. Licha ya kuelezwa kwamba Mfumko wa Bei unapungua, lakini bado tunaona fedha zetu zinapungua uwezo wa kununua bidhaa kuliko awali kadri muda unavyokwenda. Kiasi kikubwa cha fedha kinatumika katika kupata bidhaa chache. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na taasisi husika kuangalia sera zake za fedha na namna inavyoweza kuzisimamia na kuhakikisha kuwa kunapatikana unafuu katika upatikanaji wa bidhaa na huduma. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Seriakli (OCGS) kuimarisha mfumo wa utoaji wa takwimu ili zitolewazo ziwe sahihi ambazo zinaendana na hali halisi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha wananchi wa kawaida wanamudu mahitaji yao ya msingi, Kamati inasisitiza Serikali kujipangia mikakati madhubuti ya kuongeza uzalishaji wa ndani wa bidhaa za chakula zitakazotosheleza mahitaji yetu. Jambo hili pia litasaidia kuimarisha upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana wetu.

**Idadi ya Watalii waliongia Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** Idadi ya watalii waliongia nchini kwa mwaka 2021 imeongezeka kwa asilimia 51.2 na kufikia watalii 394,185 kutoka watalii 260,644 walioingia nchini mwaka 2020. Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kusimamia mikakati yake mbali mbali ya kuimarisha sekta ya utalii nchini ikiwemo mifumo ya uchukuaji wa taarifa za watalii, utaratibu wa kuchukua na kuhifadhi takwimu za mapato yanayotokana na sekta ya utalii pamoja na kuimarisha miundombinu hasa ya barabara za ndani zinazoelekea katika hoteli za kitalii.

**Usafirishaji na Uagiziaji wa Bidhaa**

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonyesha usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi kwa mwaka 2021 umeongezeka na kufikia thamani ya TZS 155.6 bilioni kutoka thamani ya TZS 65.7 bilioni mwaka 2020. Hii inatokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mazao ya karafuu na mwani. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwani imesaidia katika kuongeza mapato.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi, takwimu zinaonesha kuongezeka kutoka bidhaa zenye thamani ya TZS 847.4 bilioni mwaka 2020 na kufikia bidhaa zenye thamani ya TZS 968.6 bilioni mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Kamati inaishauri Serikali kudhibiti ongezeko la uagiziaji wa bidhaa nchini hasa

kwa zile bidhaa ambazo zinazalishwa nchini ili kutoa fursa pana kwa masoko ya ndani na kukuza biashara za wananchi wetu pamoja na kuimarisha uzalishaji wa bidhaa nchini.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022 ulijumuisha Programu 25 na miradi 39 na kupangiwa jumla ya TZS 882.8 bilioni ikiwa TZS 606.5 bilioni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na TZS 276.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Katika kipindi cha miezi tisa, Julai 2021 hadi Machi 2022, jumla ya TZS 213.0 bilioni sawa na asilimia 24 ya TZS 882.8 bilioni zilitumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati haijaridhishwa na upatikanaji mdogo wa fedha za utekelezaji wa miradi hali iliyopelekea utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa bajeti ya 2021/2022 kutofikiwa katika kiwango kinachostahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa vipindi tofauti imekuwa ikishuhudia upangaji wa miradi mingi lakini utekelezaji wake unakuwa wa kusuasua, hali inayopelekea kushindwa kupatikana kwa tija inayokusudiwa. Katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022, Programu nne (4) na miradi miwili (2) tu ya kimkakati ndiyo ilitekelezwa. Hii ni sawa na asilimia 46.1 ya miradi 13 (Programu 5 na Miradi 8) ya kimkakati iliyoidhinishwa katika mwaka 2021/2022. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali, kupanga miradi kwa mujibu wa hali halisi ya upatikanaji wa fedha ili iweze kukamilika kwa wakati na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2022

### Utekelezaji Halisi wa Mapato Julai 2021 hadi Machi 2022

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha huzingatia utekelezaji wa makusanyo ya mapato kwa miaka iliyopita. Katika kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya TZS 1,449.4 bilioni. Aidha, ukusanyaji halisi wa mapato ya Serikali kwa kipindi hicho ni jumla ya TZS 1,127.8 bilioni sawa na asilimia 78 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa upatikanaji wa mapato kwa kipindi cha miezi tisa umefikia asilimia 78 ya lengo lililopangwa, na kwa kuzingatia kuwa bajeti inayoleta tija kwa wananchi inategemea sana upatikanaji mzuri wa mapato ya ndani na ya nje, Kamati inaishauri Serikali kuendelea na usimamizi mzuri na madhubuti wa taasisi zote zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 ili mapato yaweze kupatikana kama yalivyokadiriwa na kuweza kuhudumia wananchi katika nyanja mbali mbali.

### Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha miezi tisa (9) imekusanya jumla ya TZS 8.2 bilioni kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali sawa na asilimia 52.5 ya makadirio ya TZS 15.6 bilioni. Kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakusanya na kuwasilisha mapato yake katika Mfuko Mkuu wa Serikali, Kamati inaishauri Serikali, kuzipatia mamlaka hizi fedha wanazoomba kwa wakati ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hatimae kuongeza upatikanaji wa mapato.

### Utekelezaji Halisi wa Matumizi Julai 2021 hadi Machi 2022

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonyesha, jumla ya TZS 867.6 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadario ya TZS 1,041.6 bilioni zilitumika katika kipindi cha Julai hadi Machi 2021/2022, ambapo TZS 566 bilioni ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na TZS 301.6 bilioni kwa Matumizi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuendelea na juhudi za kuimarisha mapato ya ndani ili iweze kugharamia miradi ya maendeleo kwa kiasi kikubwa na sio kutegemea zaidi mikopo au Washirika wa Maendeleo. Kwa kadri ya kiasi cha fedha kinavyokuwa kikubwa katika Matumizi ya Maendeleo ndivyo uchumi wetu utakavyoimarika kutokana na kuimarika kwa huduma za kijamii pamoja na kuimarika hali ya upatikanaji wa ajira.

**Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 136.95 bilioni, sawa na asilimia 93 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 147.98 bilioni zilitumika kugharamia shughuli mbali mbali. Kati ya fedha hizo, TZS 16.98 bilioni zilitumika kulipia marejesho ya amana za wananchi waliyoweka fedha zao katika Kampuni ya Masterlife Microfinance ltd.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapata wasiwasi juu ya matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali kuhusiana na ulipaji wa amana za wananchi walioweka fedha zao katika kampuni ya Masterlife Microfinance Ltd kwamba hakukuwa na utaratibu maalum uliowekwa wakati wa ulipaji wa fedha hizo. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu madhubuti wa utumiaji wa fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali ili kuepusha matumizi tofauti na malengo ya uanzishwaji wa mfuko huo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Serikali imetumia kiasi kikubwa cha

fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi walioweka amana zao katika Kampuni ya Masterlife, Kamati inaisisitiza Serikali kuchukua hatua stahiki kisheria kwa wahusika wa kampuni za aina hii ili vitendo vya aina hii visiweze kufanyika tena nchini.

**Mfuko wa Miundombinu**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2021/2022, jumla ya TZS 46.5 bilioni zilikadiriwa kukusanywa kutoka Mfuko wa Miundombinu, ambapo jumla ya mapato halisi yaliyopokelewa kutokana na Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha miezi 9 Julai 2021 hadi Machi 2022 yamefikia TZS 14.3 bilioni sawa asilimia 63 ya makisio ya 22.9 bilioni yaliyopangwa kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, Mfuko umetumia TZS 3.15 bilioni sawa na asilimia 7 tu ya makadirio ya mwaka kwa ajili ya kugharamia miradi mitatu kati ya miradi tisa iliyopangwa. Kamati inapata wasi wasi juu ya namna ya fedha za Mfuko huu zinavyotumika hasa ukizingatia katika utekelezaji wa miradi ambapo inakuwa chini ya matarajio ya utekelezaji wake. Hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza mfuko huu kuwa makini katika matumizi ya fedha ili kuimarisha na kutengeneza miundombinu nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa vile hadi kufikia Machi 2022, fedha zilizotumika katika Mfuko wa Miundombinu ni asilimia 7 tu ya kiasi kilichopatikana, Kamati inaitaka Serikali kuja na mkakati ambao utaiwezesha kuzitumia fedha zilizopatikana kabla ya mwaka wa fedha haujaisha. Kamati inaitanabahisha Serikali kwamba, udhaifu sio kukusanya kidogo tu bali hata kutumia kidogo kinyume na mipango tuliyojiwekea.

**Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Machi 2022, Deni la Taifa limefikia jumla ya TZS 1,202.6 bilioni ambalo limeongezeka kwa TZS 308 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 34 ikilinganishwa na Deni lililoripotiwa katika mwezi Machi 2021 ambalo lilikuwa TZS 894.6 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali pale ambapo itahitaji kukopa ili kugharamia miradi ya maendeleo, ichukuwe mikopo yenye riba ndogo na masharti nafuu pekee sambamba na kuhakikisha miradi inayotekelezwa inamaliza kwa wakati na kuwa na ufanisi ili hatimae ichochee ukuaji wa uchumi pamoja na kuongeza mapato. Aidha, ni muhimu kwa Kitengo cha Madeni kufuatilia kwa karibu takwimu zinazohusiana na Deni la Taifa ili zisaidie katika kujitathmini ukopaji wetu na namna tunavyolipa madeni hayo.

**Matarajio ya Mapato Julai 2021 hadi Juni 2022**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa mwenendo wa mapato, makusanyo yanatarajiwa kufikia TZS 1,507.0 bilioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya TZS 1,829.9 bilioni ya mwaka mzima wa fedha 2021/2022. Mapato haya yanajumuisha TZS 230.20 bilioni ambazo ni fedha za ahuweni za UVIKO 19 kutoka IMF.

**Mheshimiwa Spika,** TZS 230.20 bilioni kutoka IMF ni fedha ambazo hazikuwa sehemu ya bajeti iliyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Hivyo, kusingelipatikana fedha hizi, mapato yangelitarajiwa kufikia TZS 1,276.8 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 70 tu ya bajeti ya mwaka mzima. Hali hii inaonyesha kwamba bado utekelezaji wetu katika ukusanyaji wa mapato haujawa wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, miradi yetu ya

maendeleo imepata nguvu kwa kiasi kikubwa kutokana na kupatikana kwa fedha hizi kutoka IMF, vyenginevyo kutokana na uhaba wa mapato uliosababishwa na uwezo wetu mdogo wa kukusanya mapato tungelishindwa kutekeleza miradi hiyo. Hivyo, Kamati inaendelea kuitanabahisha Serikali kwamba bado tunayo kazi kubwa mbele yetu ya kufikia malengo ya makusanyo tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** Ili Serikali iweze kukusanya kwa ufanisi, Kamati inashauri mambo yafuatayo: Kwanza, kutatua changamoto za ukwepaji wa kodi na kupunguza upotevu wa mapato. Pili, Kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tatu, Kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija. Nne, Kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na taasisi na mamlaka mbalimbali za Serikali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua nyengine ambazo zitasaidia kuongeza mapato ni kuendelea kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji pamoja na kupanua wigo wa kodi na kujenga mahusiano na mazingira rafiki kwa walipa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati bado inasisitiza kuwekwa utaratibu maalum wa taasisi za umma kukadiriwa kiasi cha mapato yanayopaswa kukusanywa na taasisi hizo. Makadirio hayo yazingatie vyanzo vya mapato vilivyopo pamoja na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji.

**Matarajio ya Matumizi Julai 2021 hadi Juni 2022**

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Juni 2022, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia TZS 1,507.0 bilioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya TZS 1,829.9 bilioni. Matumizi ya Kazi za Kawaida ni TZS 739.0 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya kutumia TZS 947.1 bilioni na TZS 768.0 bilioni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya TZS 882.80 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inatarajia kutumia TZS 97.8 bilioni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara ambazo ni sawa na asilimia 49 tu ya makadirio ya kutumia TZS 200.2 bilioni. Aidha, kwa upande wa Matumizi Mengineyo ya Ruzuku kiasi kinachotarajiwa kutumika ni TZS 46.8 bilioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya kutumia TZS 97.5 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu hizi za matarajio zinaonyesha nakisi kubwa katika matumizi yetu hali ambayo inapelekea uzoroteshaji wa kazi za uwendeshaji wa Wizara na taasisi za umma kutokana na ufinyu wa fedha katika utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uhaba wa mapato kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo kwa kiasi kikubwa husababisha ukusanyaji hafifu wa mapato ya ndani. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali iziwezeshe taasisi kukusanya zaidi kwa kuziingizia fedha za uendeshaji wanazoomba. Aidha, Serikali iendelee kuimarisha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hususani mapato ya ndani.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, licha ya fedha zinazopelekwa katika Wizara na taasisi za umma kuwa chache,

kumekuwepo na matumizi yasiyo na tija katika nchi yetu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo: Kwanza, Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Wizara na taasisi za umma kwa kuhakikisha matumizi yote yanafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Pili, Uimarishaji wa mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato uende sambamba na mifumo ya manunuzi (e-Procurement). Tatu, Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya vipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Nne, Kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya kuanzisha miradi mipya.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kudhibiti matumizi ya Serikali, Kamati pia inaishauri Serikali kuviimarisha vitengo vya ukaguzi wa ndani vya taasisi za umma ambavyo ndivyo vyenye majukumu ya kisheria kuandaa mpango kazi wa ukaguzi, kutoa ushauri katika matumizi ya fedha kisheria, kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi pamoja na kufanya uhakiki wa vifaa vilivyonunuliwa, kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kutoa ripoti ya ukaguzi kila baada ya miezi mitatu. Kwa sasa vitengo vingi havina nguvu ya kufuatilia matumizi ya taasisi husika. Uimara wa vitengo vya ukaguzi wa ndani utasaidia taasisi husika kujifanyia tathmini zenyewe pamoja na kusaidia utendaji kazi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hilo la vitengo vya ukaguzi wa ndani vya taasisi za umma, Kamati ya Bajeti inazishauri pia Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinapofanya ziara za kukagua utekelezaji katika Wizara au taasisi za umma, ziombe ripoti za ukaguzi wa ndani za robo mwaka. Hii itasaidia kubaini kasoro za taasisi hizo katika ulipaji na ununuzi ya bidhaa na huduma mbali mbali au zinaweza kubaini udhaifu

wa Wakaguzi wa Ndani.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato katika mwaka 2021/2022, Serikali ilichukuwa hatua mbali mbali. Hatua hizo zilihusisha marekebisho ya Sheria pamoja na Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi. Kamati inaipongeza Serikali kwa zile hatua ambazo imezitekeleza kwa ufanisi na taarifa zake zilizoletwa zipo bayana na kutosheleza. Hata hivyo, zipo hatua ambazo utekelezaji wake ni mdogo au taarifa zake zilizotolewa hazijitoshelezi au zilikuwemo katika mikakati ya hatua zitakazotekelezwa lakini katika taarifa ya utekelezaji hazikutajwa kabisa. Mathalan, hatua ya Kuanza Kutoza Kodi ya Majengo (Property Tax).

### Hatua Zinazohusu Utekelezaji wa Marekebisho ya Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya utekelezaji wa baadhi ya Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria, Kamati imebaini taarifa za baadhi ya hatua hizo hazijajitosheleza. Mathalan, hadi kufikia Machi 2022, utekelezaji wa marekebisho katika Sheria ya Kampuni Namba 15 ya mwaka 2013 umewezesha kampuni 45 kutoka Tanzania Bara kusajiliwa Zanzibar. Ili uweze kupima ufanisi katika hatua hii, ilipaswa kutajwa idadi ya kampuni zote ambazo zinapaswa kusajiliwa na pamoja na lengo lilikuwa ni kusajili kampuni ngapi katika mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa utekelezaji wa hatua ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya Mwaka 2016, kumeelezwa kwamba taasisi 34 zimeunganishwa katika mfumo wa ZanMalipo. Taarifa haielezi lengo lilikuwa ni kuunganisha

taasisi ngapi. Aidha, katika hatua za utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Namba 1 ya mwaka 1995 nayo pia zimetajwa takwimu za utekelezaji uliofanyika bila ya kutajwa malengo. Kutokukamilika kwa taarifa, kunaleta ugumu wa namna kupima utekelezaji wa hatua hizo.

**Hatua zisizohusu Marekebisho ya Sheria**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa hatua za kuimarisha mapato zisizohusu marekebisho ya Sheria ambazo ni Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi, Kamati imebaini hatua ya Kuunganisha Mfumo wa TEHAMA wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania bado haijatekelezwa. Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha kwamba mfumo mpya wa Shirika la Bandari Zanzibar unaendana na mfumo wa TANCIS wa TRA.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kuendeleza Mfumo wa Kuwatambua Walipakodi Kimaeneo (Block Management System), Kamati imebaini bado mchakato wa uendelezaji wa mfumo huu unaenda taratibu mno. Kamati inashauri mfumo huu uunganishwe na Mfumo wa Anuani za Makaazi na Postikodi. Jambo hili litasaidia kuzitambua biashara zote kwa haraka kwa mujibu wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Hatua za kuimarisha mapato kwa Kuendelea na Ukaguzi wa Kodi katika Taasisi za Fedha na Kampuni za Mawasiliano haijitoshelezi. Serikali imeeleza kwamba jumla ya TZS 662.65 milioni zimekusanywa kutoka ZANTEL. Kamati ilibaini katika taarifa hiyo, hakuna maelezo ya malengo ya kiasi cha fedha kilichotarajiwa kukusanywa na pia hakuna maelezo ya kwa nini hakukusanywa mapato kama hayo katika kampuni nyengine za

mawasiliano ya simu.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza hatua ya Kuongeza Kiwango cha Gawio kutoka Mashirika ya Umma, Serikali imefanikiwa kufanya mabadiliko ya kiwango cha gawio kutoka asilimia 20 mpaka asilimia 50. Kamati inaishauri Serikali, kuyafanyia tathmini mashirika yote ili kubaini uwezo wa mashirika hayo katika ulipaji wa gawio. Serikali kupata gawio ni jambo zuri lakini umakini unahitajika kwani inawezekana baadhi ya mashirika yanaweza kudumaa iwapo viwango vya gawio vikiwa sawa. Kamati pia inaishauri Serikali kuyapitia mashirika na taasisi zote za umma na kuziimarisha kiuongozi na kiutendaji wa kisasa pamoja na kuweka mikakati mahsusi ya kuhakikisha kila shirika au taasisi ya umma inatoa gawio kwa Serikali na sio kuwa tegemezi siku zote.

## MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR KWA MWAKA 2022

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2022 yanatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 5.1 kwa mwaka 2021. Ongezeko hilo ni matokeo ya mkopo nafuu kutoka IMF na BoT, uingiaji wa watalii kwa wingi nchini, kuongezeka kwa mapato ya ndani, kuimarika kwa shughuli za uwekezaji na biashara, kuimarika kwa mifumo ya mapato na matumizi pamoja na kuimarika kwa huduma bora za viwanja vya ndege.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kwamba, Serikali isimamie mikakati iliyojiwekea katika mipango ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu sambamba na kufungamanisha ukuaji huo na uimarishaji wa hali za kimaisha za wananchi wetu.

## MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 umezingatia utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo inayojikita katika kuimarisha hali za wananchi, kukuza ajira, kuongeza uwekezaji ili kuongeza mapato ya Serikali na kuboresha huduma muhimu pamoja na ukuaji wa uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha miradi yote iliyomo katika Mpango wa Maendeleo inakuwa endelevu ili iweze kutengeneza fursa za ajira ambazo zitapunguza umaskini na utegemezi kwa kuwashirikisha wananchi katika sekta mbali mbali ili kukuza uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya TZS 1,352.19 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 ambapo ni ongezeko la asilimia 53.20 ukilinganisha na kiasi kilichopangwa kutumika kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa ongezeko hilo na kusisitiza kwamba utekelezaji wa miradi iliyopangwa ifikie malengo hatuna budi kuongeza ukusanyaji wa mapato ya kugharamia mpango huo. Serikali iweke mikakati ya kusimamia mapato kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato hususani bandarini na katika viwanja vya ndege na pia kushirikiana kwa karibu na sekta binafsi ili kuimarisha utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) katika kugharamia miradi ya maendeleo.

## MAPENDEKEZO YA MAENEO YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya maeneo ya kimkakati kwa mwaka

2022/2023 yanajumuisha kuimarisha uchumi wa buluu, kuimarisha miundombinu ya usafiri, usafirishaji na nishati, kuendeleza biashara, kuimarisha huduma za kijamii na kuimarisha utawala bora na wa haki. Kamati inaiunga mkono Serikali katika maeneo yote ya kimkakati yaliyopangwa na kuishauri mambo yafuatayo:

**Mheshimiwa Spika,** Katika eneo la uchumi wa buluu ni muhimu kwa Serikali iwekeze katika uasilia na kuyatunza mazingira ya fukwe na bahari katika maeneo yatakayo jengwa bandari za uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya usafiri, usafirishaji na nishati, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini na wakandarasi watakaopewa zabuni za ujenzi wa miundombinu hiyo. Aidha, Kamati inaisisitiza Serikali kuhakikisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi zilipwe kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kila mwananchi ili kupunguza mzigo wa ugumu wa maisha kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kuanza ujenzi wa vituo vya biashara na maonesho kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati inashauri kwamba, vituo hivyo vitakavyojengwa viwe endelevu na vitumike kimkakati kuendeleza biashara na kukuza uchumi na pato la nchi na wananchi kwa ujumla na sio kuja kutumika siku chache na baadae kutelekezwa na kupelekea fedha za walipa kodi kupotea. Aidha, Kamati inaishauri Serikali, iendelee kuwasaidia wavuvi, wakulima na wafanyabiashara katika upatikanaji wa mtaji na masoko ya bidhaa zao.

**Mheshimiwa Spika,** Kuimarisha huduma za kijamii ni jambo muhimu kwa maendeleo ya nchi, hivyo Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada za upatikanaji wa fedha zilizopangwa kwa kwa ajili ya uimarishwaji na

upatikanaji wa huduma za afya, elimu na maji ili kuharakisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki, Kamati inashauri ujenzi wa mahkama za Wilaya uanze mapema iwezekanavyo ili kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha ilizozitenga kwa ajili ya mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za kesi ili kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki sambamba na kuwa na mpango unaotekelezeka wa kusimamia haki za binaadamu.

## MAPENDEKEZO YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imekadiria kukusanya na kutumia TZS 2,590.3 bilioni, kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia 41 ikilinganishwa na bajeti ya TZS 1,829.9 bilioni katika mwaka 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Kawaida yanatarajiwa kuwa TZS 1,220.5 bilioni sawa na asilimia 47.1 ya bajeti yote na TZS 1,352.2 bilioni sawa na asilimia 52.2 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Aidha, matumizi ya Serikali za Mitaa kwa makusanyo yao ya ndani yanakadiriwa kuwa TZS 17.6 bilioni sawa na asilimia 0.7 ya bajeti yote.

**Mheshimiwa Spika,** Ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2022/2023, ni lazima ufanisi katika ukusanyaji wa mapato uwe wa hali ya juu. Hivyo, tunawanasihi wananchi wote kudai risiti za kielektronikipale wanaponunua bidhaa mbali mbali na

wafanyabiashara watoe risiti hizo pale wanapouza bidhaa zao. Aidha, tunaishauri Serikali kusimamia vyema matumizi ya fedha za umma ili sote tupate ari na hamasa ya kulipa kodi kwa hiari na hatimaye baada ya muda uwe ndio utamaduni wetu kulipa kodi bila ya shuruti. Lengo la ulipaji wa kodi kwa hiari litafikiwa pale ambapo hakutakuwa na ubadhirifu katika fedha za umma na ukitokezea wahusika wanawajibishwa bila ya muhali.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mwenendo wa hali ya dunia, Kamati inaishauri Serikali katika kubuni mikakati mahsusi ya kukabiliana na mitikisiko ya kiuchumi ya dunia inayosababishwa na vyanzo mbalimbali. Mathalan, mitikisiko inayosababishwa na vita, miripuko ya maradhi nakadhaalika.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ambalo litaisaidia Serikali kutekeleza bajeti ijayo ya mwaka 2022/2023 kwa kiwango kikubwa ni kubana matumizi katika shughuli ambazo si za msingi, ili kupunguza mzigo kwa Serikali. Kuna matumizi ambayo sio ya umuhimu sana. Unaweza kuona katika taasisi watendaji wakuu wanabadilisha samani katika ofisi zao lakini watendaji wa chini hawana vitendea kazi vya msingi kama vile kompyuta, karatasi nakadhaalika au mara nyingine utakuta katika baadhi ya taasisi, fedha zilizotumika katika posho za safari ni nyingi kuliko fedha zilizotumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za msingi za taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua nyengine ambayo Kamati inaishauri Serikali kuichukua ili kuimarisha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023 ni kuondosha vitendo vya rushwa kwenye ukusanyaji wa mapato. Vitendo vya rushwa hufanywa na watendaji wa taasisi za kukusanya kodi kwa

kukubaliana na wafanyabiashara, ili kuwakadiria kodi ya chini pale wafanyabiashara wanapokubali kuwapa rushwa, na huwabambikia kodi kubwa zaidi pale wanapokataa kutoa rushwa. Ili kuongeza ufanisi katika makusanyo, ni lazima Serikali ikabiliane kwa nguvu zote na mambo ya namna hii.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaobainika kufanya ubadhirifu katika fedha za umma nalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ijayo. Hii italeta nidhamu katika matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Kamati inaona Serikali ikijiimarisha katika ufuatiliaji wake, litaongeza mapato kwa kiwango kikubwa ni kufuatilia mapato yatokanayo na taasisi za Muungano kama vile Mamlaka ya Anga Tanzania, Mamlaka ya Kusimamia Bima Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Posta na taasisi nyengine zenye kufanana na hizo. Kwa sasa tunapata gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania tu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri pia Serikali iweke mkakati maalumu wa kufuatilia mapato yanayoweza kupatikana katika sekta ya mawasiliano. Serikali inakosa mapato mengi kutoka katika sekta hii, ni lazima utatuzi wake upatikane ili malengo yetu ya ukusanyaji mapato yafikiwe.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la mwisho ambalo Kamati inalishauri kwa lengo la kuongeza mapato yetu ni kuhakikisha kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa inainisha vyanzo vyake vyote vya mapato kwa uwazi na ukweli. Baadhi ya vyanzo huwa vinakusanywa lakini hakuna taarifa ya makusanyo inayotolewa na kuna vyanzo vyengine havikusanywi kabisa

katika baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa lakini vyanzo hivyo hivyo vinakusanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa nyengine.

## MAPENDEKEZO YA MAENEO YA VIPAUMBELE VYA KITAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imepanga kutekeleza vipaumbele sita (6) vifuatavyo:

i. Kuimarisha Huduma za Jamii,
ii. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato ya Serikali,
iii. Kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali yasiyokuwa na tija,
iv. Kuimarisha utawala bora,
v. Kuinua maslahi ya watumishi wa umma, na
vi. Kutekeleza miradi ya kimkakati.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kupatikana ufanisi na tija katika utekelezaji wa miradi ya kitaifa ni lazima kuwepo na muendelezo wa vipaumbele hivyo. Mathalan, katika mwaka 2021/2022 kulikuwepo na vipaumbele vya kitaifa kama vile kusimamia matumizi sahihi ya ardhi na kupima maeneo yote, kuendeleza utafutaji wa nishati mbadala na kuendeleza maeneo ya historia. Vipaumbele hivi vyote havipo katika muendelezo wa vipaumbele vya kitaifa katika mwaka 2022/2023. Hali inayoonyesha wazi kwamba tunashindwa kusimamia na kuendeleza mipango yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuinua maslahi ya watumishi wa umma. Aidha, Kamati

inashauri, suala la kuimarisha maslahi ya watumishi wa umma liende sambamba na uimarishaji wa uwezo wa rasilimali watu. Jambo hili litaongeza morali ya ufanyaji kazi kwa wataalamu wetu sambamba na kuimarisha uwezo wao wa kufanya kazi kwa weledi. Dunia ya sasa inahitaji weledi katika ufanyaji kazi na sio juhudi pekee.

## SHUKRANI ZA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati ya Bajeti tunamshukuru na kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kubuni na kutengeneza **Filamu ya Royal Tour.** Ni wazi kwamba, filamu itasaidia kututangaza na hatimae kuimarisha sekta nzima ya utalii pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi wetu kwa ujumla. Aidha, tunamshuruku Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kushiriki katika filamu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upekee, nachukua fursa hii pia kwa niaba ya Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Bajeti kuwashukuru Wenyeviti Wastaafu wa Kamati ya Bajeti, **Mheshimiwa Saada Mkuya Salum** na **Mheshimiwa Ali Suleimain Ameir** kwa mashirikiano yao kwangu binafsi na kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawapongeza kwa uteuzi wa nafasi zao walizozipata. Tunawatakiwa kheri na fanaka katika kutekeleza majukumu yao.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza wewe **Mheshimiwa Spika Zubeir Ali Maulid** kwa kuliendesha Baraza hili la Wawakilishi kwa weledi mkubwa. Pia

nampongeza **Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma**, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa kutekeleza vyema majukumu yake ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika.


**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inaisimamia vyema Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini wakati nilipokuwa nawasilisha hotuba hii. Matarajio yetu ni kwamba, maoni na ushauri tulioutoa katika hotuba hii utazingatiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo na sio kuchukuliwa kama ni jambo la kufuata utaratibu tu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wauchangie Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali pamoja na kuishauri vyema Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Hussein Kombo,



Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**